

# Mambo Muhimu ya Kuzingatia katika Kuanzisha Kampeni ya Kitaifa ya Kupata Huduma baada ya Kubakwa

KILA SAA  
INAYOPITA  
NI MUHIMU

Kasi ni Lazima.



Together for girls  
Ending violence against children

Unapobuni na kuzindua kampeni ya kitaifa, kuna maswali mengi ya kuzingatia katika kuandika ujumbe na utetezi. Shirika la kusaidia wasichana la Together for Girls hupendekeza kundi lako kuulizwa maswali yafuatayo:

## Ni mashirika gani yanayotoa huduma, na ni wapi?

Je, kuna mwongozo na utaratibu wakitaifa wa kufuatwa, unaojumuisha huduma kwa wasichana na wavulana? Mashirika hayo yanapokea madawa ya kutosha bila kukosekana, kama dawa za kufubaza virusi vya HIV, na dawa za dharura za kuzuia mimba? Ni huduma gani zinazotolewa mwishoni mwa wiki, na wakati wa usiku? Je, wahudumu wamepata mafunzo ya kufanya kazi na watoto?

## Je kuna huduma ya simu ya dharura ya kupata msaada kwa watoto na /au huduma ya simu ya dharura ya kutoa msaada kwa waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia?

Je, wahudumu wa ile huduma ya simu ya dharura wamepewa mafunzo ya kutoa ushauri nasaha kwa waathirika waliobakwa, na namna ya kuwaelekeza kupata huduma? Na ikiwa hakuna huduma ya dharura ya simu, kuna mfumo wa kuanzisha laini kama hiyo?

## Ni sheria zipi, sera, na utaratibu rasmi zinazohusiana na utoaji matibabu kwa waathirika baada ya kubakwa, ikiwemo zile zinazowahusu watoto, vijana, makundi madogo na makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi?

Je, wahudumu wa afya, wahudumu wa kijamii, polisi, watoaji huduma za kisheria na umma wanafahamu sheria hizo, sera na utaratibu? Ikiwa hawazijui, ni mipangilio gani ya kutoa mafunzo au kampeni za kuhamasisha unazoweza kuanzisha? Je, kuna masharti yoyote ya lazima katika kuripoti ubakaji, kwa mfano ulazima wa kuripoti kwa polisi, jambo ambalo linakuwa kikwazo?

## Ni mashirika gani ya karibu yaliyo na uwezo wa kutekeleza jukumu muhimu la kuchagiza jamii kupunguza unyanyapaa unaowafanya waathirika kuogopa kufichua visa vya ubakaji, na kuhimiza upatikanaji wa huduma kwa wanawake, wasichana na wavulana?

Ni vipi unaweza kushirikiana na makundi ya mtaani katika kuwachagiza na kuwashirikisha watu katika jamii kuhusu huduma ya baada ya kubakwa. Jambo hili ni msingi muhimu katika kufanikisha au kushindikana kwa kampeni. Kuwafikia wadau katika ngazi ya wilaya na vijijini, wakiwemo wanaotoa ulinzi, serikali za mitaa, makundi ya kiraia (yakiwemo yale ya wanawake, wanaume, na makundi ya vijana), viongozi wa kidini, machifu, washirika wa kiume, na wengineo ni jambo linalohakikisha ujumbe unawafikia wale wanahitaji kufahamu kuhusu huduma na upatikanaji wake.

## Ni njia ipi bora zaidi ya kueneza kampeni hiyo kwenye mitandao ya kijamii, na ni nani anayesikiliza?

Unapoandaa ujumbe wa mitandao ya kijamii na wa kuhamasisha watu katika ngazi ya mitaa, kukusanya makundi ya watu kwa minajili ya kupima ufuatiliaji wa ujumbe kunaweza kusaidia kuhakikisha ujumbe ulio muhimu unawafikia watu pamoja na hatua za kuchukuliwa zilizopendekezwa. Nyenzo zinazotumika kuandaa kampeni zinaweza kutayarishwa upya zikiwalenga watu wenye uelewa wa chini kama vile watoto, na watu wasiojua kusoma na kuandika.

### TOGETHER FOR GIRLS GLOBAL PARTNERS:



### EVERY HOUR MATTERS PARTNERS:



FOR MORE INFORMATION VISIT: [WWW.EVERYHOURMATTERS.ORG](http://WWW.EVERYHOURMATTERS.ORG) / [WWW.TOGETHERFORGIRLS.ORG](http://WWW.TOGETHERFORGIRLS.ORG)